

Makosa ya Kiisimu katika Filamu Fasiriwa kwa Kiswahili kutoka Kiingereza: Tafsiri ya Utokeaji wa Sauti

Ziada Tajo Ameir

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar –SUZA

Ikisiri

Wataalamu mbalimbali kama Cintaz, (1997); Luyken na wenzake, (1991) na Franco, (2001) wanahukumu tafsiri ya utokeaji sauti kuwa tafsiri rahisi, thabiti, halisi na yenye kuaminika ambayo huzuia kiwango cha kutokuaminika kutoka mazungumzo asili. Hukumu kama hiyo inaleta ukakasi kutokana na mchakato wa tafsiri. Hali hiyo imesababisha kuchunguza makosa ya kiisimu ya tafsiri ya utokeaji sauti katika filamu fasiriwa kwa Kiswahili kutoka Kiingereza. Lengo la makala hii ni kubainisha makosa mbambali ya kiisimu pamoja na kujadili sababu ya utokeaji wa makosa hayo. Data za utafiti huu zimechambuliwa kutokana na modeli ya Nord (1991). Modeli ya Nord ilijihusisha na makosa manne ya tafsiri ya matini kama vile; makosa ya kiisimu, makosa ya kipragmatiki, makosa ya kiutamaduni na makosa ya matini mahsusi. Utafiti huu uliongozwa na mkabala wa kimaelezo. Data za utafiti zimekusanywa kwa kuangalia na kusikiliza CD tano. CD hizo ni pamoja na Skip Trace, Deleted, Real Steel, Behind the Enemy line na Tiger Cage. Kwa upande wa data za lengo la pili zilipatikana kwa njia ya uchambuzi wa makala tatu. Matokeo yameonesha kwamba makosa ya kisemantiki yamechukua nafasi kubwa ukilinganisha na makosa ya kisarufi na kileksikia. Aidha, mtafiti amebaini sababu mbalimbali zilizosababisha ufanywaji wa makosa ya filamu fasiriwa kama vile tofauti za kiutamaduni, raghba ya mfasiri, msisimko wa mchezo wenyewe, uchache wa maarifa na misamiati, athari za lugha mama, ukosefu wa taaluma ya tafsiri nakadhalika. Utafiti huu umetoa mchango wa kukuza taaluma ya tafsiri katika fani ya filamu. Vilevile, umetoa mapendekezo ambayo yatapunguza makosa ya tafsiri kwa wafasiri, wanataaluma na watafiti.

Maneno Muhimu: *Tafsiri ya Uonisikivu, Tafsiri ya Utokeaji wa Sauti, Makosa ya Kiisimu*

Utangulizi

Maendeleo ya sayansi na teknolojia yameweza kuzitoa shughuli za tafsiri kutoka katika matini za vitabuni hadi katika sekta ya filamu. Hivyo, katika kipindi cha miaka ya 2000 kumekuwa na ongezeko la kundi kubwa la filamu zenye tamaduni tofauti tofauti. Kwa kiasi kikubwa filamu hizo zimechangia kuibuka kwa filamu fasiriwa kwa Kiswahili kutoka lugha za kigeni kama Kihindi, Kichina, Kiingereza, Kifilipino na lugha za Kiafrika kama Kinaijeria, Kikuyu na kadhalika. Hali hii imesababishwa na mahitaji ya hadhira lengwa ambayo ndio walengwa wa filamu hizo. Dai kama hili limethibitishwa na Cintaz na Anderman (2009, uk.4) wanaoeleza kwamba “ufasiriwaji wa programu za televisheni, chaneli na filamu unatokana na mahitaji ya hadhira lengwa kutokuwa na uwelewa wa lugha za kigeni au lugha asili”. Hoja hii imeungwa mkono na Englert (2010) anapoeleza kwamba wafasiri wa filamu hufasiri filamu kutokana na mahitaji ya hadhira lengwa na sio kwa ajili ya taifa. Aidha hoja hiyo iliendelezwa tena na Englert na Moreto (2019, uk. 272) wanaofafanua kwamba “mchakato wa tafsiri kwa wafasiri una lengo la kutoa burudani na uzoefu kwa hadhira lengwa ya Kitanzania”. Hii ina maana kwamba hadhira lengwa ndio mhimili mkuu wa msukumo wa mchakato wa filamu fasiriwa katika jamii. Ufasiriwaji wa filamu fasiriwa unatokana na tafsiri ya uonisikivu. Kundi kubwa la wataalamu wanakubaliana kuwa tafsiri ya uonisikivu ni chachu ya kukua kwa maendeleo ya teknolojia ya habari (Cintaz & Anderman, 2009; Munday, 2011; Chaume, 2013). Tafsiri ya uonisikivu imegawika katika njia tofauti. Kwa mfano, tafsiri ya usimulizi, utokeaji sauti, dabi, tafsiri ya ujumbe mfupi na kadhalika. Njia zote hizo zimefanyiwa tafiti mbalimbali zilizohusiana

na michakato, mikabala, sifa na makosa. Hata hivyo, kuna uhaba mkubwa wa tafiti za tafsiri ya utokeaji sauti. Hali hii imemsukuma mtafiti kuzamia katika kuchunguza makosa ya kiisimu katika tafsiri ya utokeaji sauti.

Orero (2009) anaeleza kwamba tafsiri ya utokeaji sauti ni mbinu ya tafsiri sauti inayotafsiriwa kwa lugha lengwa husikika sambamba na lugha chanzi. Mfasiri hupunguza sauti ya lugha chanzi ili sauti ya lugha lengwa iweze kusikika. Kwa maana hiyo sauti za lugha mbili tofauti husikika kwa wakati mmoja. Aidha, wataalamu wengine kama Brown (1993) na Kuhn na Westwell (2012, uk.446-447) wanakubaliana kwamba tafsiri ya utokeaji sauti ni msimulizi anayezungumza bila ya kuonekana katika filamu au ni sauti inayosikika lakini haitokani na mhusika yoyote anayezungumza katika skrini. Kutokana na fasili za wataalamu mbalimbali, tafsiri ya utokeaji sauti ni usikikaji wa sauti kutoka mazungumzo chanzi na kutafsiriwa kwa njia ya utokeaji sauti ya msimulizi kutoka lugha lengwa. Kwa mujibu wa Luyken, G. M., Herbst, T., Langham-Brown, J., Reid, H., na Spinhof, H. (1991), tafsiri ya utokeaji sauti ina sifa nne;

- a) Sifa ya kwanza, Isonkroni ni muda wa uanzaji wa tafsiri. Tafsiri huanza sekunde chache baada ya sauti chanzi na kumaliza pamoja au kabla ya kumaliza sauti chanzi.
- b) Sifa ya pili, Sinkronia andishi inategemea sauti chanzi iwe katika isokronia kwa sababu sinkronia andishi inahitaji sauti chanzi kusikika kabla ya mfasiri wa lugha lengwa.
- c) Sifa ya tatu, Sinkronia tendi inahusisha ni ufasiriwaji wa matukio ya mchezo katika skrini.
- d) Sifa ya nne, Sinkronia kinetiki ni tafsiri inayokwenda sambamba na matendo ya viungo vya mwili.

Dhana ya makosa katika uga wa tafsiri imejadiliwa na wataalamu mbalimbali kwa kuhusisha nadharia na mikabala tofauti. Vinay na Dalbernet (1958) ni miongoni mwa wanazuoni wa mwanzo waliojadili makosa ya tafsiri ijapokuwa hawakutoa fasili ya makosa ya tafsiri. Vinay na Dalbernet (1958) walieleza kimajumui kwamba makosa ya tafsiri hutokezea wakati mfasiri anapokosa umakini juu ya maana ya maneno tofauti yanayojitokeza katika hali ya kubadilika. Waasisi hao wameyafungia makosa ya tafsiri katika kiwango kidogo cha tofauti za maana ya maneno. Ufasiliwaji huo hautoshelezi kuelewa makosa ya tafsiri. Mtaalamu mwingine, Koller (1977) akiungwa mkono na Baker (1992) wakihusisha mtazamo wa nadharia ya uwiano wa matini chanzi na matini lengwa katika tafsiri, makosa yanachukuliwa kama kutokuwepo kwa uwiano baina ya matini chanzi na matini lengwa. Koller (1977) alisisitiza kwamba uwiano uambatane na utoshelevu wa tafsiri ya matini lengwa. Msisitizo wa Koller unatutaka kuona kwamba matini lengwa ndio kiini cha tafsiri ya matini chanzi. Wills (1982), makosa ni kwenda kinyume na kaida za kiisimu. Wilss anayaangalia makosa ya tafsiri kwa kuhusisha ukiukwaji wa kanuni katika lugha.

Hali hii inatufanya tuyaweke kando makosa yanayofanywa nje ya mipaka ya kanuni za lugha. Uwachaji wa makosa ya nje ya mipaka ya kanuni za lugha kunaweza kuathiri uwelewa mpana wa makosa ya tafsiri. Sigrid (1985) alifasili makosa ya tafsiri ni kwenda kinyume na; i) dhima ya tafsiri ii) uwiano wa matini iii) uwiano wa muundo wa aina ya matini iv) ukubalifu wa kanuni za kiisimu v) ukubalifu wa kanuni mahsusi za kiutamaduni na kihali vi) uamilifu wa mfumo wa lugha. Sigrid (1985) alikwenda mbali kiufafanuzi katika kutathmini makosa ya tafsiri. Makosa ya tafsiri hayatokani na ukiukwaji wa kanuni za lugha tu bali yanafungamana na ukiukwaji wa dhima, muundo wa matini, kanuni za kiutamaduni na kihali. Kwa mnasaba huo makosa ya tafsiri ni mwamvuli mpana unaojumuishia mambo yanayohusu lugha na mambo mengine ya nje ya lugha. Nord (1991, uk.151) “ukiukwaji wa kaida, kanuni au sheria za kimumbo”. Nord (1991) anasisitiza hayo kwa kujiegemeza zaidi na mikabala wa kiuamilifu ambapo maelezo au tamko haliwezi kuwa sahihi wenyewe lakini linatokana na ubora wa hadhira kutokana na kaida au maadili mahsusi. Kwa maneno mengine tafsiri inatokana na hadhira na kaida za jamii lengwa. Makosa ya tafsiri yanaweza kujitokeza katika aina mbambali kama ifuatavyo;

Aina za makosa ya tafsiri zimejadiliwa na wataalamu mbalimbali na kufanyiwa tathmini ya ubora wa tafsiri (TUS). William (1989, uk.23) amegawa makosa ya tafsiri katika makundi matatu; (i)

makosa hatarishi (ii) makosa makubwa (iii) makosa madogo. Nord (1991/1997, uk.75) anatafautiana na William kwa kuwa na aina nne za makosa ya tafsiri; i) makosa ya kipragmatiki ii) makosa ya kiutamaduni iii) makosa ya kiisimu iv) makosa ya matini hususi. Pym (2004) ameyagawa makosa katika aina mbili; makosa ya tafsiri yasiyokuwa sahihi na makosa ya tafsiri yenye usahihi hafifu. Hansen (2009) anatafautiana kidogo na Nord na pia anakubaliana kwa kiasi fulani kutokana na mgawanyo wake wa aina za makosa ya tafsiri. Hansen (2009) ameyagawa makosa ya tafsiri katika makundi saba. Aina hizo ni makosa ya kipragmatiki, makosa ya kiisimu matini, kisemantiki, kisimo, kimtindo, kimofolojia na makosa ya kisintaksia. Licha ya kwamba Hansen anaonekana kuwa na aina nyingi za makosa ukilinganisha na wataalamu wengine, aina zake zina muungiliano wa karibu na aina za Nord. Kutokana na hali hiyo aina saba za Hansen zinaweza kugawanywa katika aina mbili za Nord kama vile aina ya makosa ya Kipragmatiki na makosa ya kiisimu ambapo hujumuisha aina nyingine ndani yake kama makosa ya kisintaksia, kisemantiki na kimofolojia na kadhalika. Kutokana na uainishaji wa aina mbalimbali za makosa ya tafsiri, makala hii imechunguza makosa ya kiisimu kwa kujiegemeza na modeli ya Nord (1991).

Makosa ya kiisimu ni matokeo ya mapungufu katika mchakato wa kutafsiri bila ya kujali muundo wa lugha. Chandra na Wahyuni (2019) wameeleza vipengele vya kiisimu vinavyofanyiwa makosa wakati wa kutafsiri. Vipengele hivyo ni pamoja na sintaksia, mofolojia, leksikia, sarufi na fonolojia.

Aidha, watafiti mbalimbali wamefanya tafiti kuhusu makosa ya kiisimu katika tafsiri. Tafiti za makosa ya kiisimu katika tafsiri yameegemezewa zaidi katika programu za somo la tafsiri. Kuna tafiti chache zilizojikita katika kuangalia makosa katika tafsiri za filamu fasiriwa. Miongoni mwa tafiti hizo ni pamoja na Chandra na Wahyuni (2019) wamechunguza makosa ya kiisimu kwa wanafunzi wa programu ya elimu ya lugha ya Kiingereza. Watafiti hao wamebaini kosa la kileksikia limejitokeza kwa asilimia 51 kwa wanafunzi wa programu ya elimu ya lugha ya Kiingereza. Makosa mengine yamejitokeza kwa kiasi kidogo kama makosa ya kisintaksia 18%, kosa la kimofolojia 7% na kosa la kifonolojia 3.9 %.

Mtafiti mwingine, Aini (2018) amechunguza makosa ya kiisimu katika kipengele cha kisarufi. Aini amebaini kuna makosa ya matumizi mabaya ya vibainishi, vitenzi, vitenzi visaidizi, vionyeshi, viunganishi, viwakilishi na udondoshaji. Kwa upande wa Mubarak (2019) amechunguza aina mbalimbali za kiisimu zinavyotumiwa katika tafsiri ya ujumbe mfupi wa skrini kutoka katika komedi za Kiindonesia kwenda Kiingereza. Licha ya tafiti mbalimbali zilizofanywa, bado kuna mapungufu ya tafiti zilizojikita na uchunguzaji wa makosa ya filamu fasiriwa kwa Kiswahili kwa kutumia tafsiri ya utokeaji sauti.

Methodolojia

Utafiti huu uliongozwa na mkabala wa kimaielezo na kuhusisha modeli ya Miles na Huberman (1996). Data zilikusanywa kwa kupitia CD 5. CD hizo ni pamoja na *Deleted*, *Real Steel*, *Behind the Enemy line*, *Skip Trace* na *Resident Evil*. Upitiaji wa CD 5 ulimuwezesha mtafiti kukusanya makosa mbalimbali ya kiisimu. Mtafiti alitumia muongozo wa maswali wakati wa kuangalia CD. Mtafiti alizikusanya data kutoka katika MC na ML. Mtafiti alizitoa data katika mazungumzo kisha alizinakili katika maandishi. Data zilizokusanywa zilinakiliwa kutoka katika mazungumzo na kuzipeleka katika maandishi. Kisha mtafiti alizigawa data na kuzipa msimbo kutokana na aina mbalimbali za makosa ya kiisimu. Aidha, data zilihaririwa na mwisho zilitafsiriwa. Data za lengo la pili zilikusanywa baada yakupitia makala tatu ambao ni Aini (2018), *The grammatical errors in the translational text: Indonesian-english structure*; Chandra na Wahyan (2019) *Linguistic errors made by students of English Education Program in Translating Indonesian Language into English* na Putri (2019), *An analysis of types and causes of translation errors*.

Matokeo

Upitiaji wa filamu tano umewezesha kubaini makosa mbalimbali ya kiisimu. Makosa ya kiisimu yalipatikana kupitia vipengele vya kisarufi, kileksikia na kisemantiki. Aidha, imebainika kwamba makosa ya kisemantiki yamejitokeza kwa wingi ukilinganisha na makosa mengine ya kileksikia na kisintaksia.

Makosa ya Kisarufi

Makosa ya Kisarufi katika filamu fasiriwa kwa Kiswahili yalitokana na kushindwa kwa mfasiri kuhaulisha maana iliyotokana na vipengele vya kisarufi vya MC kwenda ML. Hali hiyo imesababisha kutokuwepo kwa uwiano wa matini hizo. Hayo yamethibitishwa kupitia jedwali lifuatalo;

Jedwali na. 1: Makosa ya kisarufi

Na	Matini chanzi	Matini lengwa Tafsiri ya utokeaji sauti
1	Did you see my daughter	Yupo wapi mtoto wangu
2	Let me take you to hospital	Acha mi nikupeleke hospitali
3	Help me	Jamani msaada
4	I give you the mighty Midas	Nawapatieni nyinyi bingwa Midas
5	See in TV and newspaper	Nimemuona katika televisheni na katika redio

Mifano iliyopo hapo juu imethibitisha wazi kuwepo kwa makosa ya kisarufi. Makosa ya kisarufi yaliyopatikana yalitokana na kutokuwepo kwa upatanisho wa kisarufi, udondoshaji wa vitenzi na matumizi yasiyokuwa sahihi ya kiambishi cha wakati. Kwa mfano;

Sentensi ya kwanza, Did you see my daughter = **Yupo wapi** mtoto wangu. Katika sentensi hii kuna makosa ya utumiaji usio sahihi wa kitenzi. Kitenzi **did** ambacho kinaonesha wakati uliopita kimedondoshwa. Licha ya udondoshaji wa kitenzi cha wakati, mfasiri amechopeka kiambishi **po** kinachoonessa mahali. Katika kuondosha makosa hayo, sentensi ilipaswa kuwa **ulimuona mtoto wangu wa kike?**

Sentensi ya pili, Let me send you to hospital = Acha **mi** nikupeleke hospitali. Mfasiri alitumia tafsiri sisisi au neno kwa neno. Kwa mujibu wa Tyler na McQuire (1980: 34) walitoa misingi majumui ya kutafsiri. Miongoni mwa misingi hiyo unaeleza kwamba “ a translator has to avoid translating word to word”. Hii inamaanisha kwamba tafsiri ya neno kwa neno inaweza kusababisha makosa katika mchakato wa kutafsiri. Kutokana na ufafanuzi huo, mfasiri alitumia kiwakilishi cha nafsi ya kwanza umoja **mi** sambamba na kiambishi **ni** cha upatanisho wa kisarufi cha nafsi ya kwanza umoja. Usahihi wa kuondosha makosa hayo, tafsiri ilikuwa iwe **Acha nikupeleke hospitali**.

Sentensi ya tatu, Help me = Jamani msaada. Katika sentensi hii kuna udondoshaji wa kitenzi kikuu **saidia** badala yake kitenzi kimebadilishwa na kuwa nomino **msaada**. Kwa hiyo mfasiri alipaswa kusema **Nisaidieni**.

Sentensi ya nne, Give you the mighty Midas = **Nawapatieni nyinyi bingwa Midas?**. Sentensi hii imeonesha makosa ya kiisimu. Makosa hayo yamefanyika kutokana na mfasiri kutumia tafsiri ya neno kwa neno. Jambo ambalo limeibua matumizi yasiokuwa sahihi ya kiambishi cha nafsi ya pili wingi **wa** sambamba na kiwakilishi cha nafsi ya pili wingi **nyinyi**. Usahihi wa kosa hilo, sentensi ilitakiwa iwe **nawapa Midas mwenye nguvu au hodari**.

Sentensi ya tano, See in TV and newspaper = Nimemuona katika televisheni na katika redio. Sentensi ya ML imebainisha makosa ya kiisimu baada ya mfasiri kuchepeka kiambishi **mu** cha nafsi ya tatu umoja. Kiambishi ambacho hakikujitokeza katika MC. Mfasiri amefanya hivyo kwa kuhusisha na matumizi ya picha na tukio. Mfasiri amefanya kosa hili kutokana na kushindwa kufanya uteuzi sahihi wa neno kutoka MC kwenda ML. Tafsiri sahihi ya neno newspaper ni **gazeti** na sio **redio**. Haya yamesisitizwa na Tyler na McQuire (1980) katika msingi wao unaosema “ a translator has to

select and arrange the words accurately and properly”. Mfasiri alipaswa achague neno sahihi litakalotoa maana sahihi.

Makosa ya kileksikia

Makosa ya kileksikia yametokana na mazingira ya mfasiri kushindwa kuteua neno au kifungu cha maneno chenye uwiano wa maana ya neno au maneno ya MC. Aidha, wakati mwingine mfasiri hukwepa kutafsiri baadhi ya neno au maneno. Utafiti umebaini kuwepo kwa idadi kubwa ya ukwepaji wa tafsiri ya maneno. Wakati mwingine nusu ya mchezo huwa hautafsiriwi.

Jedwali na. 2: Ukwepaji wa tafsiri

Na	Maneno kutoka MC	Hayakutafsiriwa
1	What the hell are you guys still doing here	
2	We need fresh wheel	
3	Why should me tight?	
4	Don't run from me! You can't run for me. Didi he just spit his juice in Midas face? No you didn't spit juice in Midas face. It's part time noise cras Palace. Use your left. Noisy is trying to do something with his one arm. But Midas pins him and daddy goes to work	
5	Get back on corner bitch and take this whooping like a man	

Jedwali namba 2 limeonesha maneno ambayo hayakutafsiriwa. Kutotafsiriwa kwa maneno kunaweza kutokana na mashartizuizi ya aina ya tafsiri ya utokeaji sauti. Kwa mujibu wa Luyken na wenzake (1991) wamebainisha sifa za tafsiri ya utokeaji wa sauti. Sifa za tafsiri ya utokeaji ni mashartizuizi ya ufasiri wa filamu fasiriwa. Mashartizuizi hayo ni pamoja na muda, usikikaji wa sauti ya MC na ML, usambamba wa matukio katika skrini na mwisho mfuatano wa matendo ya viungo vya mwili. Kutokana na mashartizuizi hayo, mfasiri hupata fursa ya kukuza sauti ya ML. Ukuzaji wa sauti ya ML imetoa fursa ya kukwepa kutafsiri baadhi ya maneno. Licha ya hali hiyo, hadhira lengwa hukosa fursa ya kuelewa maana kusudiwa.

Aidha, data zimeonesha kwamba mfasiri ameshindwa kuteua neno au maneno sahihi ambayo yanaendana na maana ya MC kwa hadhira lengwa. Kwa mfano, **Son of a bitch! Fuck you! Bastard! Blood fuck you!** Maneno yote hayo hufasiriwa kwa maneno mjinga au mpumbavu, ngederu, mshenzi au kulaladeki. Hali hii imetokana na tofauti za kiutamaduni kati ya MC na ML. Tofauti za kiutamaduni wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza hulazimisha mfasiri kuteua maneno yasiyoleta karaha na kukwepa maneno ya matusi. Hali hii imeelezwa na Kafipour na Jahanshahi (2015).

Vilevile, ukwepaji wa kutafsiri kunasababishwa na athari za lugha mama na tofauti za kiusuli kati ya MC na ML. Salam, Akil na Rahman (2017) wameeleza kwamba tofauti za kiusuli kati ya MC na ML huzaa makosa ya ubadilishaji wa maana ya maneno. Kutokana na sababu hiyo, wafasiri wa filamu fasiriwa kwa Kiswahili kutoka Kiingereza huamua kutumia maneno yenye kupunguza karaha na matusi au kutoyatafsiri kabisa.

Aidha, mtafiti amebaini wakati mwingine wafasiri wa filamu fasiriwa hukwepa kutafsiri baadhi ya maneno kutokana na ragha, utashi, kutojali na msimko wa mchezo wenyewe. Wafasiri wa filamu fasiriwa hujisahau kuwa wao ni wafasiri na wana dhima ya kuhaulisha ujumbe kwa hadhira lengwa. Wongranu (2017) akikazia hoja hiyo anasema kwamba, kutokujali, ukosefu wa kutokusoma, athari za maarifa ya zamani, kutokujiamini na hofu ni miongoni mwa sababu za makosa ya tafsiri.

Makosa ya kisemantiki

Makosa ya kisemantiki yamefungamana na kutokuwepo kwa usawa wa uhaulishaji wa maana kutoka MC kwenda ML. Makosa ya kisemantiki hayaepukiki kutokana na kushikamana na utofauti wa sababu mahsusi za kiutamaduni na kiisimu kati ya lugha chanzi na lugha lengwa. Makosa ya kisemantiki yaliyobainika ni pamoja na makosa ya tafsiri finyu, tafsiri tenge na tafsiri zidifu.

Makosa ya tafsiri finyu

Makosa ya kisemantiki yalitokana na ufinyu wa tafsiri. Ufinyu wa tafsiri hutokea kwa kudondoshwa kwa neno, kiwakilishi, kivumishi, kirai au sentensi nzima. Kosa hili limejitokeza kwa kiasi kikubwa katika tafsiri ya utokeaji wa sauti. Jedwali lifuatalo linathibitisha hali hiyo.

Jedwali na 3: Makosa ya tafsiri finyu

	Ufinyu wa tafsiri	MC	ML
1	kirai	Wow!, exactly, oh!, okay, bastard, Ah!, Hmm!, Hey Good time Sh!sh!sh! Hooray! Hooray! Oh! Ooh Oh ow!	

Utafiti umebaini kwamba mara nyingi wafasiri wa filamu fasiriwa hupuuza kutafsiri maneno yanayoeleza hisia za mzungumzaji wa MC. Hisia hizo ni pamoja na hisia za furaha, kushangaa, kuhusudu, hasira na huzuni. Kwa mfano, maneno kama **Wow!, exactly, oh!, okay, bastard, Ah!, Hmm!, Oh my God!, Sh!sh!sh!, Hooray! , Hooray!, Oh! , Ooh! Hooray!** na **ow!** Maneno hayo hayakutafsiriwa. Kutokutafsiriwa kwa maneno hayo baadhi ya wakati wafasiri huwa hawana uweledi wa kutosha wa kuteua msamiati unaokidhi maana ya maneno ya MC. Sababu hiyo imesisitizwa na Youfi (2014) anaposema kwamba makosa ya tafsiri hutokana na upungufu wa maarifa ya msamiati, sarufi na matumizi ya alama kutoka lugha lengwa. Pamoja na hayo, baadhi ya maneno yanaonekana rahisi na hayana umuhimu wa kufasiriwa. Wakati mwingine badala ya kutafsiriwa hutamkwa kama yalivyo katika matamshi ya ML. Kwa mfano, maneno kama **Wow!- /Waw/, okay – /okei/, Hooray! – /huraaa/, Oh!- /oh/**. Jambo hilo hutoa picha kwamba hakuna tofauti ya maneno kati ya MC na ML. Jambo ambalo sio sahihi.

Makosa ya Udondoshaji

Aidha, utafiti umebaini uwepo wa udondoshaji wa neno, au maneno au kifungu cha maneno au sentensi. Udondoshaji wa maneno unachangia kutokufikia lengo la tafsiri kwa hadhira lengwa. Jedwali na 4 linathibitisha hayo.

Jedwali na 4: Udondoshaji wa maneno

Sentensi		
	<ol style="list-style-type: none"> 1. Cause you and me we are gonna have little talk Ok. 2. Using your card. You cheat the Casino of out of a millions dollars 3. That's a lot of airline sticker and customers 4. The major shiftsform Colombia ordered our Military and diplomatic personnel 5. Why don't we meet on the ... 6. You think I will forget you 	<p>Mimi na wewe ikibidi tufanye mazungumzo Tambua kuna mabilioni ya pesa Kuna tiketi nyingi sana</p> <p>Hii ni kubwa kuliko Kolombia imeshatoa amri ya jeshi kutafuta kundi hili Kwanini tusikutane... Siwezi kukuacha hivihivi</p>

Mifano iliyomo katika jedwali imethibitisha uwepo wa udondoshaji wa maneno wakati wa mchakato wa tafsiri. Kutokutafsiriwa kwa baadhi ya maneno kunasababisha upokezi wa tafsiri isiokuwa sahihi. Tafsiri isiokuwa sahihi hupoteza lengo la tafsiri kwa HL. Kwa sababu kunakosekana kwa usawa wa tafsiri kati ya matini hizo mbili. Pia kuwepo kwa uwezekano wa hisia tofauti kwa HL (Muhammad, 2018). Kwa mfano, sentensi ya 2, udondoshaji wa maneno **Using your card. You cheat the Casino of out of...** Hadhira lengwa hupokea ujumbe usiokuwa sahihi. Jambo ambalo halikubaliki. Kwa sababu lengo la tafsiri ni kufikisha ujumbe uliosahihi. Hali hii inachangiwa na kutokujali kwa mfasiri wa ML. Wongramu (2017) anathibitisha kwamba makosa ya tafsiri hutokana na uzembe au kutokujali kwa mfasiri. Kutokujali kwa mfasiri kunatokana na usomaji mbaya wa MC. Hii inamaanisha kwamba wafasiri wa filamu fasiriwa huwa hawajali kama tafsiri zao ni sahihi au la au zina utoshelevu wa kimaana au la. Hali hiyo imejirejea kwa mfano wa tatu na wa nne.

Makosa ya uziada

Makosa ya uziada yanatokana na upachikwaji wa maneno au uongezwaji wa neno au maneno kinyume na mazungumzo ya MC au bila ya mazungumzo MC. Jedwali lifuatalo linathibitisha hali hiyo.

Jedwali na. 5: Makosa ya uziada

Uziada	MC	ML	Uziada
Neno	1. Help me,	Jamani msaada,	Jamani
Kirai	2. What have you done first periods	Ulikuwa unafanya nini, biashara gani miaka ya nyuma?	Biashara gani miaka ya nyuma?
Sentensi	3. See my lawyer 4. Oh! My oh!you think I will forget you. You are my friend	Jamani nataka kumuona mwanasheria wangu mbona mnaninyima haki Oh!mtu wangu, mtu wangu wa nguvu. Unajua mimi na wewe ni marafiki. Siwezi kukuwacha hivihivi	Jamani, mbona mnaninyima haki mbona mnaninyima haki Siwezi kukuacha hivihivi
	5. Who kill my son?	Sasa naomba uniambie nani aliyeniulia mtoto wangu?	

Sentensi Na. 1 na 3 zimeonesha uziada wa neno **Jamani**. Uziada wa neno **Jamani** unatokana na athari ya lugha ya kwanza. Mfasiri ametumia uzoefu wa matumizi ya neno hilo katika jamii yake. Aidha, sababu ya athari ya uzoefu wa lugha mama imeweza kujitokeza tena katika mfano wa 4. Mfasiri ametumia uzoefu wa maneno ya mitaani kama **mtu wangu wa nguvu** au **mtu wangu wa ukweli**. Kosa hilo la uziada linasaidia HL kufahamu kwa urahisi kilichokusudiwa.

Sentensi Na. 2, 3 na 4 zina uziada wa tafsiri unatokana na muendelezo wa mazungumzo ya MC. Mazungumzo ambayo HL haiwezi kuyasikia. Kwa mfano, **biashara gani miaka ya nyuma?**, **mbona mnaninyima haki** na **Siwezi kukuacha hivihivi**. Uziada wa sentensi hizi umesaidia kujenga muktadha uliokusudiwa na kurahisisha mawasiliano kwa HL. Aidha, matokeo yameonesha kwamba kuna uziada wa tafsiri bila ya mazungumzo MC. Uziada wa tafsiri hufanywa kutokana na raghba ya mfasiri au msisimko wa mchezo wenyewe. Hali hii humsukuma mfasiri kuongeza mazungumzo, kutoa komenti ya jambo, kutabiri matukio, kutia vionjo mbalimbali na uhusishaji wa mandhari ya jamii lengwa. Pamoja na hayo, uziada hufanywa kutokana na ufasiriwaji wa matendo na picha bila ya kuzingatia mazungumzo ya MC. Kwa mfano,

1. Kila mtu aliingia na Roboti wake.

2. Wako na Roboti hapa ndo habari ya mjini
3. Roboti wenyewe ana kiduku
4. Kazi kazi tu. Unyama ni mwingi sana jioni ya leo balaa ndo kwanza linaanza. Wacha tuangalie nani zaidi.
5. Inabidi amtafute yule alomuua bwana. Anaonekana kama jenerali wa Kolombia. Ilibidi aje mpaka hospitali kufanya ujanja, kavaa vazi kama daktari. Katafuta jina ndo huyu hapa. Kuna ulinzi akajua ndo hapa hapa. Kacheza na huyu jamaa fasta. Baada ya mazungumzo wanaume ikabidi watimke zao.

Ushahidi wa sentensi za hapo juu zimefasiriwa kutokana na matendo na muonekano wa picha. Uziada wa namna hiyo huzuia kupatikana kwa maana ya asili ya MC kwa HL. Ijapokuwa kwa upande mwingine huamsha hisia kwa HL.

Utenge wa tafsiri unasababishwa na ufahamu mbaya wa maneno kutoka MC au tofauti za kiutamaduni kati ya MC na ML. Kwa mfano,

1. Real steel - chuma cha kweli
2. But your government **blaming** us they are calling us assassins - serikali yako **imeplani** jambo hilo kwa muda mrefu kutuita sisi wauaji.
3. The government will **discredit** me and call me a **liar** - serikali **itamchukulia** kama **mnawabadilikia**.
4. The priority is my **men** - uwezekano ni **vijana wangu**
5. Unless you want to be **resigned** to cell in Leavenworth- **nimekwambia** ufanye ulivyoambiwa ufanye huwezi kufanya kitu tofauti
6. Yeah well I can not **contradict** them -n siwezi kwenda **kutoa ushahidi**
7. Get up! Twende juu
8. I **didn't care** **sijamuona**
9. I **say nothing** **sijaona** chochote
10. The priority is **my men** uwezekano wangu ni **vijana wangu**
11. Buda I **kill you with a gun** Buda **mshenzi huna akili**.

Sentensi Na. 1, 2, 3, 4, 5 na 6 zimeonesha utenge wa tafsiri uliosababishwa na ukosefu wa uwelewa wa maneno kutoka MC. Kwa mfano, neno **Real** = **ukweli**. Neno **Real** haliendani na neno chuma. Badala ya kutumia neno ukweli, mfasiri angepaswa atumie neno halisi = **chuma halisi**. Mfasiri alitumia neno **ukweli** kutokana na uzoefu wa maarifa ya awali aliyokuwa nayo. Hata hivyo, mfasiri ameshindwa kutumia kamusi katika kupata maana ya msingi ya neno. Hali hiyo imeweza kujitokeza katika mifano mingine kama **blaming** = **imeplani** badala ya **imelaumu**, **discredit**= **itamchukulia** badala ya **itanidharau**, **resigned**= **nimekwambia** badala ya **kujiuzulu na contradict** = **kutoa ushahidi** badala ya **kupingana**. Baker (1992) anasema kwamba kadiri ya lugha mbili zinapokuwa tofauti ndivyo makosa mengi hujitokeza. Maelezo ya Baker yanatupa maana kwamba wafasiri wa filamu fasiriwa hufanya makosa ya tafsiri kutokana na tofauti za kimsamiati na vipengele vyengine vya kiisimu. Licha ya sababu hiyo, wafasiri wa filamu fasiriwa wakati mwingine hushindwa kutumia vizuri makamusi. Silalahi, Rafli na Rasyid (2018) wanaunga mkono sababu hiyo. Silalahi, Rafli na Rasyid wamesisitiza kwamba, wafasiri wasipotumia vyema makamusi au tafsiri za kieletroniki husababisha kufanya makosa.

Sentensi ya Na.9 na 11 zimeonesha utenge uliosababishwa na uzembe au kutojali kwa mfasiri wa ML. Wangranu (2017) amekuja na mtazamo kwamba uzembe katika tafsiri unatokana na usomaji mbaya wa mfasiri, kuingiliwa na maarifa ya zamani, kutokujiami na wasiwasi. Kwa mfano, I say nothing = **sijaona chochote** na Buda I kill you with a gun = **Buda mshenzi huna akili**. Mifano ya sentensi hizo zimeonesha utenge mkubwa ambao umeweza kupotosha maana na lengo la kimawasiliano la MC. Kutokana na hali hii, HL haitaweza kupokea tafsiri sahihi.

Sentensi Na. 7 na 10 zimeonesha makosa yanayotokana na tafsiri ya picha na matendo. Kwa mfano, neno Get up! = **twende juu**. Mfasiri alitafsiri kutokana na kitendo cha roboti kushindwa kusimama juu. Vilevile, neno the priority is my men = uwezekano wangu ni vijana wangu. Mfasiri alifasiri neno **men** kwa maana ya vijana kutokana na hali ya kimuktadha.

Hitimisho

Kwa ujumla dhana ya makosa ni dhana majumui. Umajumui wa dhana ya makosa unatokana na kufungamana kwake na nadharia na mikabala mbalimbali. Kutokana na mfungamano huo, makosa ya kiisimu ya tafsiri ya filamu fasiriwa kwa Kiswahili yaliyobainika ni pamoja na makosa ya kisarufi, makosa ya kileksikia na makosa ya kisemantiki. Kwa upande wa makosa ya kisarufi imebainika kutokuwepo kwa upatanisho wa kisarufi, udondoshaji wa vitenzi, matumizi yasiokuwa sahihi ya kiambishi cha wakati. Makosa haya yamesababishwa na masharti zuizi ya tafsiri ya utokeaji sauti, sababu za kiutamaduni na ukosefu wa maarifa yaliyosababisha uteuzi mbaya wa maneno. Kwa upande wa makosa ya kileksikia kuna makosa ya kutokutafsiriwa kwa baadhi ya maneno, kutafsiriwa kwa kupunguza makali ya maneno na kubadilisha maana ya asili ya MC. Makosa haya yamesababishwa na sababu za tofauti za kiutamaduni, athari za lugha mama na kutojali kwa mfasiri. Makosa mengine yaliyojitokeza ni pamoja na kosa la kisemantiki. Kosa la kisemantiki limetokana na kuwepo kwa tafsiri finyu, tafsiri ya uziada na tafsiri tenge. Sababu kuu zilizosababisha makosa hayo ni athari za lugha mama na ufahamu mbaya wa maneno.

Ufanyaji wa makosa katika tafsiri ni jambo lisiloepukika. Kwa sababu shughuli ya uhawilishaji wa matini mbili tofauti sio jambo rahisi. Pamoja na kuwepo kwa ufanyaji wa makosa mbalimbali ya ufasiri wa filamu fasiriwa kwa Kiswahili makosa hayo yanaweza kuepukika. Kwa kiasi fulani tunaweza kupunguza makosa ya tafsiri katika filamu fasiriwa kwa wafasiri kuzipitia kazi zao baada ya kuzitafsiri, kutumia vizuri visaidizi vya kazi zao kama matumizi ya makamusi, kuwa na ujuzi wa fani ya tafsiri, kuwa na uwelewa mpana na uweledi wa utamaduni na vipengele vya kiisimu vya MC na ML.

Marejeleo

- Aini, N. (2018). The grammatical errors in the translational text: Indonesian- English structure. *Tell Journal*. 6(2), 55-61.
- Baker, M. (1992). *A Coursebook on Translation*. Routledge.
- Brown, L. (ed.) (1993). *The new shorter Oxford english dictionary*. Clarendon Press.
- Chaume, F. (2012). The turn of audiovisual translation: New audiences and new technologies. *Translation spaces*, Vol (11), 105-123. https://www.researchgate.net/publication/262946400-John_Benjamins_Publishing_Company
- Chandra, J and Wahyuni, I. (2019). Linguistic Errors made by students of English Education Program in Translating Indonesian language into English. *Advances in Social Science, Education and Humanities Research*, Volume (411), 343-350.
- Englert, B. (2010). In need of connection: Reflections on youth and the translation of film in Tanzania. In Stichproben. (Eds.), *Journal of African Studies*, 137-159. Wiener Zeitschrift für kritische Afrikastudien/ Vienna.
- Englert, B. & Moreto, Ng. (2010). Inserting voice: Foreign language film translation as a local Phenomenon in Tanzania. In K. Balogun, L. Gilman, M. Graboyes, & H. Iddrisu (Eds.). *Journal of African Media Studies*. DOI: 10.1386/jams 2 .2.225-1
- Englert, B. & Moreto, Ng. (2019). Retelling the World in Swahili Revisiting the Practice of Film Translation in Tanzania. <https://www.researchgate.net/publication/348900247>
- Franco, E. (2001). Voiced-over television documentaries. Terminological and conceptual issues for their research. *International Journal of Translation Studies*. 13(2), 289–304
- Hansen, G. (2009). A Classification of Errors in Translation and Revision. In H. Lee- Jahnke, P. A. Schmitt & M. Forstner (Eds.) *In Enhancing Translation Quality: Ways, Means, Methods* (kk313–327). CIUTI-Forum

- Miles, M. B. & Huberman, A. M. (1994). *Qualitative Data Analysis: An expanded Source book (2nd ed.)*, Sage Publications, Inc.
- Kafipour, R., & Jahanshahi, M. (2015). Error Analysis of English Translation of Islamic Texts by Iranian Translators. *Journal of Applied Linguistics and Language Research*, 2(3), 238-252.
- Koller, W. (1971). *Katharina Reiß: Möglichkeiten und Grenzen der Übersetzungskritik*. Hueber.
- Kuhn, A & Westwell, G. (2012). *A dictionary of film studies*. Oxford University Press.
- Luyken, G. M., Herbst, T., Langham-Brown, J., Reid, H., & Spinhof, H. (1991). Overcoming Language Barriers in Television: Dubbing and subtitling for the European audience. European Institute for the Media.
- Mubaraki, Aishah. 2019. Representation and Subtitling of Linguistics Varieties in Egyptian Films. Doctoral Dissertation. Leeds: University of Leeds.
- Muhammad, H. A. (2018). *Semantic loss in Translating movie subtitles from English into Kurdish*.
- Munday, J. (2011). *Introducing translation studies; Theories and applications*. Routledge.
- Nord, C. (1984/1991/1997b/2005). *Text Analysis in Translation: Theory, methodology, and didactic application of a model for translation-oriented text analysis*. Rodopi.
- Orero, P. (2009). Voice-over in Audiovisual Translation. In J. D. Cintaz & A. Ramael. (Eds.) *Audiovisual Translation: language Transfer on screen* (kk. 130-139). Palgrave Macmillan.
- Putri, T. A. (2019). An Analysis of types and causes of translation errors. *Etnolinguist*, 3 (2), 93–103.
- Pym, A. (2004). On the pragmatics of translating multilingual texts. *The journal of specialized Translation*. Issue (1). 14-28.
- Rahmatillah, K. (2013). Translation errors in the process of translation. *Journal of English and Education*, 7 (1), 14-24. <https://www.researchgate.net/publication/312526464>
- Salam, Z. M., Akil, M., & Rahman, A. Q. (2017). Translation Errors Made by Indonesian-English Translators in Crowdsourcing Translation Application. *ELT Worldwide*, 195-204.
- Sigrid, K. (1985). The problem of translation error evaluation. Translation in foreign language Teaching and Testing. In T, Christopher, A. E. Hieke. (Eds.). *Translation in Foreign Language, Teaching and Testing*, 169-179. Narr
- Silalahi, M., Rafli, Z., & Rasyid, Y. (2018). The Analysis of Errors in Translation of Scientific Text from English to Indonesian Language. *Journal of Eductaion, Teaching, and Learning*, 3(1), 23-27.
- Utami, S. (2017). The Source of Errors in Indonesian-English Translation. *Jurnal KATA*, 1(2), 192-202.
- Vinay, J., & Darbelnet, J. (1958/1995). *Comparative Stylistics of French and English*. John Benjamins.
- Williams, M. (1989). The Assessment of Professional Translation Quality: Creating Credibility out of Chaos. *Translators' Journal*. 2(2), 13-33. <http://id.erudit.org/iderudit/037044a>
- Wills, W. (1982). *The Science of Translation: Problems and Methods*. Gunter.
- Wongranu, P. (2017). Errors in Translation Made by English Major Students: A Study on Types and Causes. *Kasetsart Journal of Social Sciences*, 117-122.
- Yousofi, N. (2014). Describing the Errors in the Translations of Iranian Novice English Translators. *Procedia - Social and Behavioral Sciences*, 1952-1958.